LIDEMO.NET
LÍNGUAS DE MOÇAMBIQUE

# WAZILI-ILAHI

**Ficha Técnica**

Título: Wazili-Ilahi
(O Messias)
(The Christ)

Língua: Kimwani

Primeira edição electrónica, 2010

Produzido por: JUWA (Associação Jumuliya ya Wamwani)
lidemo.net@gmail.com
C.P. 652
Nampula, Nampula
Moçambique

O utilizador pode copiar e distribuir a obra.

wakwanza, wanafunzi-wo wasa manyumba awo, wawasa wawa zawo, wasa vinu piya, ipate wanfulate Insa. Akulazimisha uwe unfulate, unkubali iye, ulipeleke kwake iye. Iye alazimisha vinu piya. Íkiwa Insa Wazili-Ilahi kawa sawa-sawa na caalitula kuwa-co, vyalazimisha iye ndi vyakweli-kwelini. Iye aalandanisiwa na kiyumbe asaka kuwa wonse, katika kupongoliwa kwake, mainsha ake saana dambi, mazina ake, usemi wake, uwezo wake nkulu, kutabika kwake, pamoja na kifo cake. Iye kawankuwinshi mpaka lelo; iye kawa pamoja na wale wamwamini iye. Awalebelela mbinguni piya wenye kunfulata iye. Akúja suku kalibu. Hapana mwengine tena wakulingana na Insa, sibinguni wala simulumwengu-mu. Ntamana iye alazimisha kuwa nfalume na Bwana nkati ya mainsha ako.

**9. Uwazani kuhusu Insa pasaka kuludila tena mulumwengu-mu?**

Insa aludila tena mulumwengu-mu. Iye mwanyewe kakikisha kinu kamba eci. (Yáhaya 14:1-3)
Na malaika newo novyo wakikisha kuwa iye aludila tena mulumwengu-um. (Vitendo 1:11)
Piya Maklishtãu kaanuni wankunlidila Insa. Anta maisilamu wakwijiwa kuwa Insa akuja kutawala. Iye akuja kuwatwala wafulatani wake wakawe naye pamoja mbinguni. Insa akuja kutawala ulumwengu nzima-wu ; iye nfalume wa ulumwengu-wu. Insa akúja kuwashinda maaduwi wake piya.

Wanu wengine wakwamba Insa akúja kutawala myaka alubaini fala Mwenyezimungu kasema kuwa akúja kutawala myaka elufu. Omi nikubali vyaamba Mwenyezimungu. Ndi kweli, Insa áludi; nowo wakati-wo, wanu piya wakúja kwakikisha kuwa: “Insa Wazili-Ilahi ndi nfalume wa mafalume, na mwenye wa mamwenye.” Uwe ukuja kwimila mbele yake ; iye ndi âja kukulamula. Wakati wausaka kufika mbele yake, akudaili: “Uwazani kuhusu omi-pa?”, ukúja kunjibu kinani?
Ukamba: “Uwe kuwa nabii”, uhukumiwa konta iye aalandanisiwa na munu. Iye tu basi ndi Nvushi, bola zaida ya nabii mmojiwapo.

Nani âja kuludi kuja kutawala? Nabii Musa? Nabii Ibulahima? Nabii Daudi? Nabii mwengine mmojiwapo? Anta! Bwana Insa akúja na akuwa mwenye kulamula shaliya. Mwenyezimungu kawolotela piya wanu ewu ukweli-wu kwa kunfufula Insa ka wafwi. Iye akúja, na kila munu akúja kunshuhudiya. Iye aapo wakunlandanisa.

**10. Uwazani kuhusu vyalazimisha iye?**

Insa kaamba:

> “Njooni kwangu omi umwe piya wenye kusokela na wenye kukunishiwa mashaka, omi nukupani pumuzi!” (Matwaya 11:28)

Iye lelo kawankukwita. Wakati wawetile wanafunzi wake



# Wazili-Ilahi

**Uwazani kuhusu Wazili-Ilahi, Al-Masih?**

Malafiki zangu, mumwijiwa Al-Masih wawenye-yu?

Metílo a “Al-Masih” luga ya kiyalabu sawa-sawa na usowezi wa kiyeblaniya “Mashiah” na usowezi nkizungu wa “Messias”. Basi, “Al -Masih” na “Messias” kinu kimoja noco, akwambiwa munu mmoja noyo, Nabii Insa. Sambi, noci ceo ca “Messias”, maana ake kinani? Iye nKolowani akwitiwa “Al-Masih” fala aisema maana ake. Bibiliya (Tauleti na Zabuli pamoja na Injili) eci ceo-ci awapo maana ake.

Nkati ya shaliya ya Musa, Mwenyezimungu kashulutisa kuwa wanu wa kutawaziwa kutenda vinu takatifu wajuzi wamiminiliwe mafuta. Jambo-li loolota kuwa Lohõ Takatifu wa Mwenyezimungu amwijala munu atondoliwe ipate azidi kupewa uwezo atimize nafsi ya Mwenyezimungu. Noli jambo-li likitendiwanga daima-zi pawakitawaziwa walongozi wa dini ponse, minabii pamoja na mafalume wa Izilaeli. Visemiwe mBibiliya (kwa nfano, Daniyeli 9:25,26 na Zabuli 2:2) vyolota kuwa munu mmojiwapo maalumu pakulu akúja kulamusa ufalume wa Mwenyezimungu. Visemíwe vile vibushuliwa tangu mida kuhusu ceo cake na wakati wasaka kuja. Aje etiwe “Atawaziwe”, kwa luga ya waeblaniya ísema “Mashih”. (“Masih”) Wakati wajile Insa, Mayahudi wengi wammanyila kuwa Wazili-Ilahi ndi ile amiminiliwe mafuta akimwijala Lohõ Takatifu ipate awavushe wanu madambi awo.

Mbibiliya kitabu ca Injili, Insa kadaili javi: “Muwazani kuhusu Wazili-Ilahi?” (Matwaya 22:42) Na iye mpaka sambi-pa akudaili uwe: **Uwe uwazani kuhusu Wazili-Ilahi?** Piya íbidi majibu ako uwe mwanyewe, konta majibu ako uwe ndi kupeleka kaili ladi yako konse mainsha ako a lelo na maala kauka kuinshi mbele yako daima milele.

## 1. Kuhusu kupongoliwa kwake ka maajuza, uwe uwazani?

Aapo munu mwengine tena apongoliwe kamba vyapongoliwe iye. Iye ndi Insa, mwana wa Maliyamu. Sambi, uwe umwita Sumaila ‘mwana wa Ibulahima’, Yáhaya ‘mwana wa Zakaliya’, Muhammad, ‘mwana wa Abdulah’. Wanu wengine piya wakwitika na mazina a wawazawo. Sababuni Insa kwitika na zina la mamaye? Konta awele na wawaye mwanadamu! Kapongoliwa na mwali wa bikila! Iye kapongoliwa kwa uwezo wa Mwenyezimungu (kwa kudula ya Mwenyezimungu) bila kwingila mwanadamu kati-kati. Myaka miya saba (700) ipitile nyuma sanapongoliwa Insa, Nabii Izaya kâsema namuna vyaaja kupongoliwa:

> “Basi, Mola mwanyewe akúja kukwisusilani alama: Mwali wa bikila akwimita,  ampongola mwana nlume na zina lake akúja kwitiwa Emanuweli, maana ake ‘Mwenyezimungu kawa pamoja nofwe.’” (Izaya 7:14)

Na vikuna novyo-novyoni kamba vyâsemile - fyoma habali kamba eyi mBibiliya, Matwaya 1:18-25.

Mwenyezimungu kamumba Adamu, wawa yetu, kamumba kwa utope wa aldhi, na ofwe piya tiwa wanawe Adamu anta na minabii neyo piya. Ofwe tumbiwa kwa aldhi, fala Insa kesuka mbinguni. Iye kâwa swafi na kasitawi kamba maji a nvula akulawa julu. Wanu wengine piya wawa kamba utope: wanyata, awali swafi, awejala madambi. Tifyoma kuwa Insa kâja mulumwengu kuwavusha wenye madambi. (1 Timotiyu 1:15) Ofwe tipongoliwa mulumwengu nomu, fala iye kesusiwa na Mwenyezimungu kaja kutivusha. Bibiliya ísema: “Tangu mwanzo ákiwapo ile etiwa Usemi”. (Yáhaya 1:1) Insa ákiwa Usemi ile na mpaka lelo iye ndi Usemi nowo. Kalipindula mwili wake kawa mwanadamu.

> “Tangu mwanzo ákiwapo iye etiwa Usemi. Iye kwa kuwa Usemi kawa pamoja na
> Mwenyezimungu, na Usemi-wo úkiwa wa Mwenyezimungu



## 8. Uwazani kuhusu kubanziwa kwake?

Mbibiliya, nkati ya kitabu ca Vitendo vya Mawalii, tifyoma javi:

> “ …kabanziwa wakinang’aniza javi, na likisuka wingu likinfinika. Ewo wakinang’aniza julu novile lungu-lungu akibanziwa akúka, we! Mpunde noule walawilila wanu wawili na mavazi melupa-vu, wakiwadaili: ‘Umwe, wanu wa inti ya Galileya, mbana munan’ganiza julu lungu-lungu? Noyu Insa wamumonile akibanziwa akúka binguni, aludi kamba vyamumonile akikwela novyo.’ ” (Vitendo 1:9-11)

Na nkati ya walaka ya Wafilipi, tifyoma javi:

> “Insa daima kawa sawa-sawa na Mwenyezimungu.
> Fala aasakile kulisukuza noyo haki ya kuwa sawa-sawa na Mwenyezimungu-yo. Kwasa javyo, kwa kusaka kwake mwanyewe, kasa piya haki zake, kalitula kuwa ntumisi, kalitula kuwa sawa na wanadamu. Kwa kuinshi kamba mwanadamu, kalinyenyekeya kamwinshimu Mwenyezimungu mpaka kufwa kwake pansalaba. Ntamana Mwenyezimungu kankulisa Insa ishima zake pakulu pawenye, na kampa zina bola zaida ya mazina mengine, ipate kwa inshima zake piya viyumbe wamwabudu Insa: viyumbe vya binguni, viyumbe vya duniya, na viyumbe vya kuzimu.” (Wafilipi 2:6-11)

Ninadaili kipinga kimojiwapo ca Mayahudi, “Nani ájuzi kutukuziwa pakulu binguni?”, piya nanga wanijibu: “Musa”. Kinu kimoja noco nikiwadaili Waisilamu, nanga wanijibu: “Muhammad”. Nikiwadaili wenye kunfulata Insa, nanga wanijibu: “Insa Wazili-Ilahi”. Fala Mwenyezimungu andailile munu mawoni, iye katolotela mwenye ubola pakulu: iye kampa Insa inshima zaida ya viyumbe piya ipate viyumbe piya vinsujudile Insa.

fala kanywa yake aambule.
Kanyamala kamba mwana wa kondoo oka kusinjiwa,
au kamba kondoo pasinjiwa mabululu ...
Kalaviwa mulumwengu mwawainshi wanu-mu
kwa sababu ya dambi za wanu wetu,
ingawa tangu aatupile shaliya ;
nkanywa mwake aalawile masemo a ulongo …
Iye kapeleka mainsha ake awenye,
Iye kawasa maaduwi wake wantabisha kamba kisomi ;
fala iye kalitika mizigo ya dambi za wanu wengi,
kawalebelela duwã wakintabisha wale waswamiiwe.”
(Izaya 53)

Aanafwa munu tangu namuna vyafwile Insa. Iye aalandanisiwa na munu mwengine tena.

**7. Uwazani kuhusu kushinda kashindile kifo?**

Insa kafwa na kazikiwa. Maaduwi wake watenda juhudi-zi piya kuwa Insa asilawe nkabuli mule.
Wâtula liwe likulu panlyango wa kabuli, wâziwa na wazunguliza masuludadu. Fala novyo sivyo, iye kafufuka na kalolota hai mbele ya wanafunzi wake. Ewo wankumbula, walya na wanywa naye. Iye kawolotela vijalãa vya mmakono na mmaulu mwake. Kwa suku moja kalolota mbele ya wanu zaida ya miya ntanu. Kwa kufufuka kwake, Mwenyezimungu kawolotela wanu wankubali Insa, kafala yatendile iye mala moja kwa daima.

Kifo ndi aduwi nkulu. Uwe ukufwa, nomi novyo nikufwa. Minabii wafwa na kila mmoja kawa nkabuli mwake mpaka lelo-vi. Fala alihamduli-llahi, Insa kashinda kifo! Insa hai mpaka lelo na kawanawo uwezo wa kuwavusha piya wanu wóka upande wa Mwenyezimungu kwa njila yake iye. Insa tu basi ndi afufuke kwa milele nkati ya wafwi. Iye aalandanisiwa na munu mwengine.



Iye tangu mwanzo kawa pamoja na Mwenyezimungu.
Julu ya Usemi, Mwenyezimungu komba vinu piya.
Iye acipo kinu combile bila Usemi …
Iye etíwe Usemi kalitádula kawa mwanadamu, kainshi nofwe.”
(Yáhaya 1:1-3, 14)

Wanawalume wawili safali moja wagwilila mpondo la kwica. Mmoja ile kamwambila mwenziwe: “Nilavye maala mwa kofya-mu, mwijala utope munyata”.
Mwenziwe ile akinjibu: “Uwe kuwa tolu! Nukuvushaja nili hali yauli noyo?”
Wó wawili wale wekala mpondo mule, hapana wa kunvusha mwenziwe.
Ikisa wasikila shauti julu na wawona nzizi ukisusiwa. Ewo wakijuzi wavushiwe na munu sagwilile mpondo mule. Neyo munu-yo kaja kwa kusaidiiwa ka julu noko.
Mwanadamu bola pakulu nkati ya minabii piya aakidili kutivusha tilawe mpondo la dambi. Fala Insa anta dambi yakupongoleliwa noyo awele nawo. Iye kesuka mbinguni.

Mwenyezimungu kawapeleka malaika kuja kweleza kupongoliwa kwake, konta kasiyana na wanu wengine piya. (Fyoma Matwaya 1:20 na Luka 2:9) We! Piya-ya ndi matajabisani! Anamba kupongoliwa tangu mwananlume javyo kamba vyapongoliwe iye. Vyapongoliwe iye, kapongoliwa neye tu basi. Iye aalandanisiwa na munu mwengine.

**2. Uwazaja kuhusu namuna zake?**

Iye kákamilika. Tangu-tangu aakolile dambi na anta mala moja aakosile. Ntamana aimbidile kulebela nswamaa. Kila munu mwenye kumopa Mwenyezimungu, ájuzi anze kukubali kuwa kakosa ikisa alebele nswamaa ka Mwenyezimungu. Ibulahima kakubali makosa ake na Daudi novyo kakubali makosa ake. Minabii piya wakijuzi wakubali makosa a dambi zawo. Uwe ukisakula mBibiliya au munsuwafu, ausingana nsitali mmojiwapo wa kusema kuwa Insa kâlebela nswamaa ka Mwenyezimungu. Iye aasakula nswamaa konta

awele na dambi. Ailini mwenziwe maalumu kandika: “Iye aakolile dambi, wala nkanywa mwake aalawile masemo a ulongo.” (1 Pedulu 2:2) ; na mwenziwe mwengine kandika: “Iye aana dambi.” (1 Yáhaya 3:5) Pedulu na Yáhaya wamwijiwa sana-sana Insa, visitoshe ewo wakikisha kuwa iye aana dambi!

Mwenyezimungu kaswamii minabii wakati wawakubalile dambi zawo, fala Insa asakule kinu kamba eco konta awele na dambi. Visitoshe, iye kâwadaili maaduwi wake: “Pamuli-po nani akidili kwákikisha kuwa omi niwa nawo dambi mmojiwapo?” (Yáhaya 8:46) Aalawilile anta aduwi wake mmoja wa kumolota kwamba kakola dambi mmojiwapo nkati ya mainsha ake. Ofwe-pa nani shalati ayelela kundaili aduwi wake javi?

Insa vyâlongopeliwe ka Pilatu nfalume wa shaliya víkiwa vyaulongo anta na Pilatu noyo, awonelele kosa limojiwapo likulu lakutenda iye, ntamana akililavya munkonjo akámba: “Omi-pa siina lawama julu ya kufwa kwake eyu munu-yu.” (Matwaya 27:24) Tangu anaalawilila munu saana dambi. Iye kawa yeka yake tu basi wala alandanisiwa na munu mwengine tena.

**3. Uwe uwonaja kuhusu usemi wake?**

Wakati mwengine maaduwi wake wakiwapeleka masuludadu wanfunge. Masuludadu wale wakinsikiliza vyaakifunda, wakiludi sawanfungile, wakamba kwa kutajabu: “Vinu vyasowele eyu mwananlume-yu aapo manzilo asowele tangu!” (Yáhaya 7:46)

Tulani kuwa vyakweli, iye kaamba:

> “Omi ndi nulu ya kuwamwalikila wanu mulumwengu-mu.
> Akilawilila munu wakunifulata, apata nulu ya kulimwalikila
> namuna ya mainsha kamili, enenda tena nkisi.” (Yáhaya 8:12)

Suku moja nkulungwa mmoja kasema: “Minabii íwa kamba mwezi. Mwezi uwala usiku. Minabii ija na nulu ya Mwenyezimungu



Iye tangu âkiwa saanakola dambi, ntamana aalazimishiwe kufwa. Iye nanga kabaziwa binguni safwile, fala kahitali kufwa kwa mema a wanu wengine. Kapeleka mainsha ake kwa sababu yetu ofwe. Kafwa ipate ofwe tiswamiiwe madambi etu. Kafwa kwa sababu yako uwe. Nsunga mwema kapeleka mainsha ake kwa sababu ya makondoo ake.

Nabii Daudi na nabii Izaya pamoja na minabii wengine wasowela tangu mida kuhusu kufwa ka Insa. Kwa nfano, nabii Daudi kasema javi:

> “Mmakongolo munisuluka,
> lilimi linipala kumalada,
> kunefya pansi kunitipuka mwa maiti.
> Cinizunguliza kipinga ca wabaya,
> wanifulata kamba umbwa.
> wanibâula mmaulu na mmakono.
> Makongolo angu piya awalangika,
> maaduwi wangu waninang’aniza, wakinishupa.
> Mavazi angu watongelana watupu,
> anzu yangu watendela kula.”
> (Zabuli 22:14-18)

Nabii Izaya kasema javi:

> “Akikejeliwa na akishupiwa pakulu zaida ya wanu wengine,
> mwenye kuhitamili …
> Kweli-kwelini iye kasukula uzuni wetu na malwazo etu ;
> na ofwe tikinnang’aniza tikidaniza kuwa kawanawo uzuni,
> wa kulumiziwa na kutabishiwa na Mwenyezimungu.
> Fala iye kalumiziwa kwa sababu ya dambi zetu,
> ofwe tivushiwa kwa hukumu zimpatile iye,
> ofwe tiponesiwa kwa kwibiiwa kwake.
> Piya-fwe tikenendanga kamba makondoo wakwasika ;
> kila mmoja akukilila njila yake ;
> fala Mwenyezimungu kantika iye dambi zetu piya-fwe.
> Iye wantabisha na wantenda kila hukumu,

mainsha mapya, mainsha a milele. Iye akidili kupindula mainsha ako ikiwa kunlebela. Uwazani kuhusu uwezo wa matajabisa ake? Iye kawanawo uwezo piya, aapo mwengine wakumpunda iye.

**6. Uwazani kuhusu mashaka ako?**

Uwazani kuhusu kifo cako?
Ukwijiwa ndepi kauka kufwila? Kuno aula inti nyengine?
Ukufwa nsafali au ukufwa pakinanda nnyumba mwako?
Ukwijiwa namuna vyauja kufwa? Ukufwa ku ulwele au ajali namuna nyengine?
Ukwijiwa kusema suku yauja kufwa? Uinshi myaka myengapi?
Mwakani, mwezini, sukuni yauja kufwa?
Kusema kweli, ofwe atijiwa suku ya cija kifo. Ila Mwenyezimungu tu basi ndi ejiwa.

Fala Insa ákijiwa piya kuhusu kufwa kwake, na kabula ya kukuna kàsema ndepi, mwaja na sukuni yaaja kufwa. (Luka 18:31-33) Iye mbele ákija kufwa kamba: "Kondoo wa Mwenyezimungu apelekiwe kuja kuwalavya wanu madambi mulumwengu-mu!" (Yáhaya 1:29) Iye akuja kufwa wakati mmoja nowo Mayahudi pawatenda shelehe ya kusinja kondoo kushehelekela Pashukwa.

Insa kâwambila kuwa akúja kufufuka suku ya tatu. Na kweli-kwelini vikuna kamba iye vyambile. Iye akijiwa sana-sana, awele kamba wanadamu wengine. Minabii awejiwe suku ya kufwa, nofwe novyo atijiwa suku yatisaka kufwa, tifwila-pi, tifwa mwaja na sukuni Mwenyezimungu yatulile.

Fala Insa kaamba:

> "Baba wangu anipenda, konta niwa tayali kulipeleka kufwa ipate niludile kuinshi tena. Hapana alavya mainsha angu bila hiyala yangu ; omi mwanyewe ndi nilavya hiyala ya kufwa kwangu. Omi niwanawo haki ya kulipeleka kuulaiwa na haki ya kuludila kuinshi tena upya." (Yáhaya 10:17, 18)



mulumwengu mwakwinukala-mu. Mwezi uwa kamba nabii. Mwezi úwala, úwala pakulu mpaka utenda tumba, ikisa ukúka ukisa aba-aba, mwinsho auwoneka tena. Falakini uwe usangaike konta úwoneka mwengine, newo úwala novyo kamba vyaukiwala wisile-wo. Kwa namuna moja noyo, minabii ndi vyawakilawilila novyo, akilawilila mmoja, akipita, akija mwengine. Kila nabii keleza habali zake, kafwa kamwasila nabii mwengine."

Dini ya wanadamu sawa-sawa na nlangaza wa mwezi au wa kandiyelu. Falakini nani halisi asakula nlangaza ntoto kamba ewo nakwanza kulawa juwa?

> Insa kaamba: "Omi ndi nulu ya kuwamwalikila wanu mulumwengu-mu."

Iye kawa kamba juwa. Juwa tangu alipunguka wala alifwa. Madambi etu na kutowa kwetu kunkubali Mwenyezimungu ndi kamba mawingu vyakingiza juwa, fala juwa latámba kuwa liwa kamba Insa anta likingiziwe alasa kuwala kanguvu zake na utukufu. Insa kaja ka wanu piya wa mataifa piya.

Iye kaamba tena: "Omi ndi njila ya ka Mwenyezimungu, ndi ukweli wa Mwenyezimungu na ndi niwápa wanu mainsha kamili. Njila yúka ka Baba ndi nomi tu basi, aipo namuna nyengine tena ya kúka ka Baba." (Yáhaya 14:6)
Minabii ikúja ikiwolotela wanu njila ya kuludila kuwa pamoja upande wa Mwenyezimungu. Ewo wamba: "Eyi ndi njila ya Mwenyezimungu. Tendaci, fulata evi vyaufulata-vi. Fulata ezi amuli-zi." Fala Insa kaamba: "Omi niwa njila. Nifulate."

Suku mmoja nnemba mmoja akipita akenenda kaya ulu, akasika. Iye akilawa kaya nyengine na aakijiwa kusowela sana luga ya noile kaya yôkile ile. Iye kandaili pulisiya njila ya kúka kâfikile. Pulisiya ile kanjibu javi: "Fulata eyi balabala-yi, mbele-ko ukapite balabala nyengine ya nkono sonto, ikisa uzungunuke ukilile upande wa nkono nlilo. Ukiluke ntado, ikisa uke na balabala noyo mpaka panyumba ya golofa upande wankono sonto."

Nnemba ile pawonile javile akanza kulila, pulisiya ile kamwambila sana-sana njila ile fala nnemba ile kâsokela-sokelanga ntamana aakidilile kufulata mwambiliwe mule piya. Kwa noule upande ule, kâlawilila mwananlume wa kwao kumoja, nnemba ile akikoliwa nkono sana-sana akilongoziwa kunyumba yâfikile.

Wakati nnemba ile wásokele, kwa kuwa aakikidili kwenenda, mwananlume mwengine ile kampinga mpaka kunyumba yâfikile. Pulisiya ile **kamolotela** njila fala mwananlume mwengine ile kantenda kuwa **ndi** njila yawenye. Insa kaamba: “Omi **niwa** njila yakúka ka Baba.”

Uwe uwazani kuhusu hadisi zake za matajabisa? (Kwa nfano, fyoma Luka 15) Kuhusu talifu yake ngema, uwe uwazani? Iye kaamba: “Njooni kwangu omi, umwe piya wenye kusokela na wenye kukunisiwa mashaka, omi nukupani pumuzi!” (Matwaya 11:28)

Uwazani kuhusu usemi wake? Aanalawilila munu asowele kamba iye, aapo wakunlandanisa iye mulumwengu-mu wala mbinguni.

**4. Kuhusu mazina ake, uwazani?**

Minabii wengi wawenye wawanawo mazina maalumu kuhusu cawajilile. Kwa nfano, Ibulahima akwitiwa “ lafiki wa Mwenyezimungu”. Insa akwitiwa “Usemi wa Mwenyezimungu” na “Mwana wa Mwenyezimungu”. Sambi munu akwajibiwa pakulu na lafiki yake zaida mwanawe? Iiii, sivyo! Na mBibiliya tifyoma: “Eyu mwanangu wa kunajibu; iye insikilizeni.” (Luka 9:35)
Kwa kunmanyila Insa ka piya minabii wengine Mwenyezimungu kamwita mwanawe. Kinani Mwenyezimungu cakisaka kusema?
Ofwe tikwamba kuwa mwana anlanda wawaye, na patimmona Insa, ndi patimwijiwa kweli-kwelini Mwenyezimungu. (Wona Yáhaya 14:9) Mwana kawanawo haki ya kwitika zina la wawaye, kanawo nafasi ya kusowela kwa zina la wawaye. Eci ndi caatendile Insa wakati wâkiwa mulumwengu-mu. Ndi ntamana akitiwa “Usemi wa



Mwenyezimungu”. Mwenyezimungu kasowela kwa njila yake. (Wona Waeblaniya 1:3) Zina la Insa bola pakulu, alilandanisiwa na zina la munu mwengine.

**5. Uwazani kuhusu uwezo wake?**

Iye atenda piya. Iye kawanawo uwezo na mamulaka piya. Nani akidili kúwapa mainsha wafwi? Ila Mwenyezimungu basi. Nani akidili kuwaponesa wanu wakulemala? Ila Mwenyezimungu basi. Nani akidili kuwaponesa vipofu? Ila Mwenyezimungu basi. Na Insa katenda piya-vi. Kaponesa kila aina ya ulwele-u piya. Aapo anta nlwele mmojiwapo wantuwise bila kumponesa. Iye kawatuwisa mashetwani na usemi mmoja tu basi. Iye kapindula mainsha a wanu mpaka kawanusulu madambi awo.

Minabii wengi pamoja na wanu wa Mwenyezimungu watenda maajuza na waponesa kwa zina la Mwenyezimungu, fala Insa aatendile matajabisa kwa zina la Mwenyezimungu, ila daima-zi kwa uwezo wa nguvu zake iye mwanyewe, na kwa zina lake iye mwanyewe. Kwa nfano, iye kamwambila mwananlume wakulemala: “Uwe nukwambila, lamuka, sukula kinanda cako-co, uke kwenu.” (Luka 5:24) Na mwananlume ile akitenda novile-novileni.

Insa aampele munu tiba anta mala moja, kawaponesa wanu kwa uwezo wake na zina lake. Mwananlume wakwitiwa Lazalu kafwa, wanzika, na wamwitisa Insa. Paajile Insa, ili kuwa Lazalu tangu akafwe zipita suku nne. Insa akúka kukabuli kwake, akamba: “Lazalu! Njoo kuno! Lawila panja-pa!” (Yáhaya 11:43) Iye akilawa nkabuli mule. Insa kolota sana-sana kuwa ákiwa na uwezo wa kuwafufula wafwi. Iye kaamba: “Omi ndi ile awafufula wanu ka wafwi na kuwapa uhai.” (Injili ya Yáhaya 11:25)

Ífika suku wafwi piya wakúja kusikila shauti ya Insa. Na uwe, íkiwa kufwa, noyo suku-yo ukúja kufufuka. Na wakuja kufufuka Musa na Ibulahima pamoja na minabii piya. Fala kwa sambi nopa, Insa ákupa